**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**652** **ELIMU KWA MICHEZO**

**Muda: Saa3 Hours** **Mwaka: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa ufupi dhana
   (a) **Rasilimali katika michezo**

   (b) **Aina za rasilimali katika michezo**

2. Eleza kwa kifupi michezo minne ya asili inayofundishwa shuleni.

3. Pendekeza hatua nne zitakazotumika katika kukimbia na kuruka wakati wa kufunga goli katika mpira wa kikapu.

4. Ainisha sheria nne zinazotakiwa kuzingatiwa katika mchezo wa tenesi.
   Mpira unapigwa mara moja tu kabla haujagusa ardhi mara mbili upande wa mchezaji anayepokea.

5. Fafananua stadi nne za mchezo wa mpira wa netiboli.
   Stadi ya kupokea mpira ni uwezo wa mchezaji kuweza kupokea mpira kutoka kwa mchezaji mwenzake kwa mikono miwili au moja kwa usalama.

6. Eleza kwa kifupi faida nne walizopata vijana baada ya kujitolea kusimamia shughuli za mashindano ya michezo ngazi ya kanda.

7. Chambua stadi nne muhimu katika mpira wa mikono.

8. Bainisha faida nne ambazo nyanja ya michezo inapata kutokana na teknolojia ya mawasiliano.

9. Eleza kwa kifupi mambo muhimu ya kuzingatia ili kufanya maandalizi ya kufanikisha ligi ya kijiji.

10. Chambuan njia nne za mawasiliano katika michezo.

11.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Tumia hoja tano kueleza sababu ya nchi nyingi barani Afrika kuweka kipaumbele katika michezo.

12. Fafanua hatua tano za muhimu za kumpatia huduma ya kwanza mwanafunzi aliyepata ajali ya kuanguka uwanjani.

13. Chambua kwa kina makundi matatu ya mifumo ya mpira wa miguu.

14. Taja kanuni sita za usalama zinazopaswa kuzingatiwa katika michezo ili kupunguza ajali na kuipunguzia shule gharama.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org